JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

RUWASA

**20/05/2024**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wa Wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma kwa niaba ya Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo nafasi za kazi **ishirini na nne (24)** kama ifuatavyo;-

## 01. MSIMAMIZI MKUU WA CHOMBO CHA UTOAJI HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII (SUPERVISOR) – NAFASI 8

**Sifa za Mwombaji:-**

- Awe Mtanzania mwenye Akili timamu anayejua kusoma na kuandika
- **Elimu;** Awe na elimu kuanzia Kidato cha Nne na kuendelea
- **Ujuzi;** Awe na Cheti cha Ufundi Sanifu level III, Astashahada au zaidi kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali
- Awe na uwezo wa kufanya kazi pamoja na kusimamia mafundi wasaidizi
- Awe na umri kuanzia Miaka 18 hadi 40
- Awe Mwadilifu, Mwaminifu na hajawahi kushtakiwa kwa Makosa ya Jinai
- Awe na uwezo wa kutekeleza majukumu yake pasipo kusimamiwa pamoja na kusimamia waajiriwa wengine wote wa Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii
- Awe na uzoefu usiopungua Mwaka mmoja katika Fani aliyosomea (Uzoefu wa kusimamia Miradi ya Maji ni sifa ya ziada)
- Awe na uwezo wa kutumia Kompyuta
- Awe tayari kufanya kazi katika kituo chochote cha kazi atakachopangiwa

## MAJUKUMU YA MSIMAMIZI MKUU WA CHOMBO

- Atakuwa ndiye mtendaji/msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO)
- Atakuwa ndiye Katibu wa Kamati (Bodi) ya Maji ya Chombo
- Atafanya kazi chini ya usimamizi wa Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO)
- Atasimamia utoaji huduma ya maji yenye ubora kwa wateja/wananchi
- Atasimamia watumishi wengime wa Timu ya uendeshaji
- Ataandaa taarifa/ripoti zinazohusu uendeshaji wa Chombo za wiki, mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima na kuziwasilisha kwa Kamati ya Maji ya Chombo
- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Chombo ikiwa ni pamoja na Mapato na Matumizi
- Kuhamasisha uchangiaji wa huduma ya maji
- Kutatua na kusuluhisha migogoro baina ya wateja na Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji
- Kufanya manunuzi ya mahitaji ya Chombo kwa kufuata taratibu za manunuzi ya Umma
- Kuweka na kutunza kumbukumbu zote zinazohusu uendeshaji na matengenezo
- Atatoa taarifa kwa Kamati ya Maji kuhusu mahitaji ya rasilimali watu (wa muda maalumu au wa kudumu)
- Ataweka malengo ya utendaji kwa ajili wa watumishi (timu ya uendeshaji) na kufanya tathmini ya kila mara
- Kuandaa taarifa za Uendeshaji wa Chombo za Wiki, Mwezi, Robo mwaka, Nusu Mwaka na Mwaka kisha kuziwasilisha katika Vikao vya Kamati ya Maji ya Chombo na kwa Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Kondoa
- Kupanga na kusimamia Bajeti ya Uendeshaji, Matengenezo ya Skimu na kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalamu kwa Kamati ya Maji na Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Kondoa.
- Kusimamia Mapato na Matumizi ya Ankara za Maji

- Kupokea maelekezo na Ushauri wa Kitaalamu toka kwa Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Kondoa
- Kuwasilisha Miongozo ya Kitaalamu kwa Kamati ya Maji.
- Kuhamasisha Uhifadhi na Utunzaji wa Miundombinu ya Maji na Vyanzo vya Maji.
- Awe na uzoefu usiopungua Mwaka mmoja katika Fani aliyosomea (Uzoefu wa kusimamia Miradi ya Maji ni sifa ya ziada)
- Awe na uwezo wa kuendesha pikipiki na awe na leseni

**02. FUNDI MSAIDIZI WA CHOMBO CHA UTOAJI HUDUMA YA MAJI NGAZI YA JAMII – NAFASI 8**

**Sifa za Mwombaji:-**

- Awe Mtanzania mwenye Akili timamu anayejua kusoma na kuandika
- **Elimu;** Awe na elimu kuanzia Kidato cha Nne na kuendelea
- **Ujuzi;** Awe na Cheti cha Ufundi Sanifu level I - III, kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali
- Awe na umri kuanzia Miaka 18 hadi 40
- Awe Mwadilifu, Mwaminifu na hajawahi kushtakiwa kwa Makosa ya Jinai
- Awe na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa wakati pasipo kusimamiwa
- Awe na uwezo wa kutumia Kompyuta
- Awe tayari kufanya kazi katika kituo chochote cha kazi atakachopangiwa
- Awe na uwezo wa kuendesha pikipiki na awe na leseni

**MAJUKUMU YA FUNDI MSAIDIZI**

- Atawajibika kwa Msimamizi Mkuu wa Chombo
- Kufanya matengenezo ya miundombinu ya skimu pale ambapo kuna hitilafu;
- Kudhibiti upotevu wa maji kwa kuhakikisha anagundua sehemu zinazovuja na kudhibiti
- Kuwaunganishia maji watumiaji maji na kuhakikisha anawafungia mita
- Kuhakikisha anadhibiti maunganisho ya maji kinyume na utaratibu
- Kuweka kwa wakati rejesta ya rasilimali na kitabu cha kumbukumbu ya matengenezo

- Atafanya kazi zingine zote atakazopangiwa na Msimamizi Mkuu wa Chombo

## 03. MHASIBU WA CHOMBO CHA UTOAJI HUDUMA NGAZI YA JAMII - NAFASI 8

**Sifa za mwombaji:-**

- Awe Mtanzania mwenye Akili timamu anayejua kusoma na kuandika
- **Elimu;** Awe na elimu kuanzia Kidato cha Nne na kuendelea
- **Ujuzi;** Awe na Astashahada ya Uhasibu au zaidi
- Awe na umri kuanzia Miaka 18 hadi 40
- Awe Mwadilifu, Mwaminifu na hajawahi kushtakiwa kwa Makosa ya Jinai
- Awe na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa wakati pasipo kusimamiwa
- Awe na uwezo wa kutumia Kompyuta
- Awe tayari kufanya kazi katika kituo chochote cha kazi atakachopangiwa
- Awe na uwezo wa kuendesha pikipiki na awe na leseni
- Awe na uwezo wa kuandaa taarifa za fedha na kutunza Vitabu vya kumbukumbu za fedha (Cash Book, Ledger, Receipt Book, Hati za Malipo, Reconciliation n.k)
- Awe na uwezo wa kutumia Komputa

**MAJUKUMU YA MHASIBU WA CHOMBO**

- Atakuwa diye msimamizi wa masuala ya kifedha katika Chombo cha Utoaji Huduma Ngazi ya Jamii
- Kusimamia ukusanyaji wa malipo ya Ankara za maji
- Kuandaa Bajeti ya mwaka ya CBWSO
- Kuandaa taarifa zote za kifedha na kuziwasilisha kwa Msimamizi Mkuu wa CBWSO
- Kufanya malipo baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa CBWSO na Meneja wa RUWASA Wilaya
- Kutunza vitabu vya fedha, hati za malipo, nyaraka za Manunuzi na nyaraka zote za uthibitisho wa mapato, malipo na matumizi ya fedha ya shughuli husika
- Kupeleka fedha zote Benki za makusanyo ya Ankara za maji kabla ya matumizi
- Kushauriana na Msimamizi Mkuu wa Chombo katika masuala yanayohusu fedha katika kutekeleza shughuli zote za Chombo

- Kupokea na kutekeleza maelekezo yote toka kwa Mtendaji/Msimamizi Mkuu (**Supervisor**) wa Chombo
- Kuandaa na kusimamia Bajeti za Uendeshaji na Uwekezaji mdogo wa Mradi.
- Kutoa tafsiri ya Miongozo ya Fedha kwa Msimamizi Mkuu (**Supervisor**) na Kamati ya Maji
- Kusimamia Taratibu, Kanuni, Miongozo na Sheria za Fedha za Umma.

**MASHARTI YA KAZI**

- Kazi itakua ya mkataba wa kipindi cha miaka mitatu. Mkataba unaweza kuhuishwa na mwajiri ambaye ni Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO) kutokana na utendaji kazi mzuri wa mhusika.
- Malipo ya mshahara kwa mwajiriwa yatatokana na makusanyo/ mauzo ya maji ya Chombo
- Mwombaji awe tayari kufanya kazi katika CBWSO yoyote atakayopangiwa katika Wilaya ya Kondoa

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA**

i. Maombi yote yaambatane na vivuli vya vyeti vya Masomo, Mafunzo, Wasifu Binafsi (**CV**) ukionesha wadhamini watatu.
ii. Muda wa kupokea maombi ni ndani ya **Siku Kumi na Nne (14)** kuanzia tarehe **21/05/2024** hadi tarehe 0**3/06/2024**, Saa Tisa na Nusu Alasiri (**09:30 Alasiri**).Maombi yatakayowasilishwa baada ya muda huo hayatapokelewa.
iii. Waombaji wote waweke Namba za Simu/Barua pepe(E-mail) kwenye Barua za Maombi ya kazi, Majibu yatatolewa kwa njia ya Simu na Barua pepe (E-mail) kwa wote watakaoitwa kwenye Usaili.
iv. Waombaji waweke picha ndogo (**Passport size**) moja ya rangi iliyopigwa hivi karibuni katika barua za maombi ya kazi.
v. Barua za Maombi ya kazi ziandikwe kwa Mkono
vi. Maombi ya kazi yanaweza kutumwa kwa **barua pepe**; **kondoadm@ruwasa.go.tz** Au yawasilishwe kwa mkono kwa kuletwa moja kwa moja katika Ofisi ya Meneja wa

RUWASA Wilaya ya Kondoa zilizopo jirani na Benki ya CRDB Tawi la Kondoa ama zitumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;-

MENEJA WA RUWASA (W),
RUWASA
S.L.P 85.
**KONDOA**

Tangazo hili limetolewa na:-

*Mhandisi Majid A. Mtili,*
**MENEJA WA RUWASA (W)**
**KONDOA**

MENEJA WA RUWASA
KONDOA